## OFISI YA RAIS TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARI MWAHU

S.L.P 261

KATESH –HANANG

25/11/2022

**Kumb. Na. MWH/F1/2023/01**

JINA LA MWANAFUNZI

S.L.P ________________________

KATESH–HANANG

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA –2023 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWAHU.</u>**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari MWAHU mwaka 2023, ambayo ipo umbali wa km 30 magharibi kusini mwa mji wa Katesh katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Usafiri wa basi kutoka mji wa Katesh kuja Mwahu unapatikana katika kituo cha mabasi Katesh kwa nauli ya tsh. 2000/=.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 09/01/2023 na hivyo mtaanza kuripoti shuleni siku ya Jumatatu tarehe 9/01/2023, na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2023.

### 1.0MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

#### 1.1SARE ZA SHULE

#### A: SARE ZA WASICHANA

- Sketi mbili za rangi ya jani la mgomba (Kiwe kitambaa cha Material namba 1)
- Sketi ziwe ndefu chini ya magoti, ziwe rinda box
- Shati mbili nyeupe aina ya tetroni zenye mikono mifupi
- Sweta la rangi ya jani la mgomba.
- Viatu vyeusi ngozi visivyo na visigino wala urembo vya kamba



Edit with WPS Office

- Soksi ndefu nyeupe (Jozi mbili).
- Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo
- Fulana (T-shirt) za rangi ya bluu bahari na sketi ya rangi hiyohiyo kwa ajili ya michezo
- Aidha anaweza kuja pia na Track suit za rangi ya blue-nyeusi michirizi ya rangi nyeupe kwa pembeni kwa matumizi ya michezo ya aina mbalimbali.
- Wanafunzi wa Kiislamu wavae hijabu za rangi nyeupe juu ya sare za shule au hijabu za rangi nyingine juu ya sare za michezo.
- Tai ya rangi nyekundu.

**B: SARE ZA WAVULANA**

- Suruali mbili za rangi ya jani la mgomba zenye rinda mbili kila upande zisiwe mnyonyo au "model" na ziwe za kitambaa kizito namba moja.
- Mashati mawili meupe ya tetroni mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo visigino virefu wala urembo na vyenye kamba.
- Bukta za bluu na T-shirt ya kijani kibichi kwa ajili ya michezo
- Tai ya rangi ya nyekundu.

**1.2VIFAA VYA DARASANI**

- Daftari kumi na moja (11) aina ya counter
- Kalamu ya wino na penseli
- Mkebe wa hesabu (Mathematical set)
- Mfuko wa kubebea madaftari au begi
- Dictionery ya English –English au English – Swahili.

**1.3MAHITAJI MENGINE**

- Aje na jembe jipya lenye mpini imara kwa wavulana na Kwanja jipya kwa wasichana.
- Aje na ndoo moja au mbili kwa matumizi yake (kwa wale wa hosteli).



Edit with WPS Office

- Aje na sahani mbili au sahani moja na bakuli kwa ajili ya matumizi ya chakula
- Aje na kikombe kwa ajili ya uji.
- Aje na ufagio wa chelewa kwa ajili wa usafi.

### 1.4 CHAKULA CHA WANAFUNZI

- Kikao cha wazazi kwa pamoja kilipitisha na kuelekeza Kamati ya Chakula iliyoundwa na kikao cha wazazi ikusanye michango ya chakula kwa muhula kama ifuatavyo:–

| AINA YA MICHANGO | WANAFUNZI WA KUTWA | WANAFUNZI WA HOSTEL |
|---|---|---|
| A: NAFAKA MAHINDI | DEBE 2 | DEBE 4 |
| B:NAFAKA MAHARAGE | DEBE 1 | DEBE 2 |
| C:FEDHA | 58,500/= | 88,500/= |
| D: MENGINEYO | | |

**NB**: (i)Nafaka ziletwe shuleni siku ya kuripoti au kabla.
(ii) Fedha zinawekwa benki ya NMB au kwa wakala wa Benki ya NMB aliyeko karibu yako.

- Namba ya Akaunti ni **41010006364**
- Jina la Akaunti ni **KAMATI YA CHAKULA MWAHU SEKONDARI.**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE YA SEKONDARI MWAHU

**3.1** Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

**3.2** Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

a) Heshima kwa viongozi wa nchi, walimu,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri kwa kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu

**c)** Kuheshimu **NEMBO,NYIMBO, BENDERA, PICHA ZA VIONGOZI WA TAIFA NA FEDHA ZA TAIFA.**

d) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya(matusi) kwa mwalimu, watumishi wasio



Edit with WPS Office

walimu, wageni na wanafunzi wenzake

e) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wewe kuwa mwanafunzi katika shule hii.

g) Kutunza usafi mwili na mazingira ya shule

h) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa

i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

j) Kunyoosha mkono na kusimama pindi unapouliza au kujibu swali

k) Kutoa taarifa ya afya yako bila kuficha jambo lolote

l) Kuheshimu mahali pa kulia chakula (bwalo) vyumba vya madarasa,ofisi, mali za umma na za binafsi

**m)** Kuheshimu na kutekeleza sheria nyingine zozote ndogondogo utakazo zikuta shuleni, na viongozi wa **SERIKALI YA WANAFUNZI**

**3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

❖ Wizi

❖ Uasherati na Ushoga

❖ Ubakaji

❖ Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, mirungi, kuberi n.k

❖ Kupigana au kupiga

❖ Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

❖ Kudharau bendera ya Taifa

❖ Kuoa au kuolewa



Edit with WPS Office

- Kupata mimba/ kusababisha mimba, kuharibu mimba ndani na nje ya shule
- Kutoa mimba
- Kugoma, kuchochea na kuongoza kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Mwanafunzi kumiliki/kuwa na simu ya mkononi.

Karibu sana.

................

Ezekiel M. Kulunya

Mkuu wa shule.



Edit with WPS Office

**PRESIDENT’S OFFICE –REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MWAHU SECONDARY BSCHOOL –MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To be completed by Medical officer in a Government hospital in respect of all new entrants to Mwahu sec school.

Full name. ……………………………………………………………………

Age ………………………….

1. Blood count (red and white ) ………………………………………
2. Urine examination. …………………………………………………
3. Stool examination …………………………………………………..
4. Syphilis test …………………………………………………………..
5. T.B Test……………………………………………………………..
6. Eye Test ……………………………………………………………….
7. Ears Test ……………………………………………………………….
8. Spleen ………………………………………………………………..
9. Abdomen ……………………………………………………………….
10. Chest test ……………………………………………………………….
11. Additional Information or any other physical , mental, hereditary, or infectious diseases

    ………………………………………………………………………………………………………………………

    ………………………………………………………………………………………………………………….

    Treatment after examination………………………………………………………………..

    **MEDICAL CERTIFICATE**

    I Certify that above mentioned has been examined and found fit to pursue for further Education



Edit with WPS Office

Signature …………………………………………..Designation ………………………………………..

**FOMU NA. 4.** TAREHE.................................

**FOMU YA MAPOKEZI YA MWANAFUNZI SHULUENI.**

**SEHEMU A:**

**IJAZWE NA MWANAFUNZ**

1. Jina la mwanafunzi (majina matatu)..........................................................
2. Taifa ....................................................................................................................
3. Tarehe ya kuzaliwa.......................................................................................
4. Shule anayotoka...........................................................................................
5. Tarehe ya kutoka Shule hiyo....................................................................

**SEHEMU B:**

**IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

1. Jina la mzazi/mlezi (majina matatu).................................................................................
2. Simu ya mzazi/mlezi....................................................................................................
3. Mahali anapoishi (kata)...............................................................................................
4. Kazi ya mzazi/mlezi........................................................................................................
5. Mahali anapofanya kazi..............................................................................................

**NDUGU WAWILI WA KARIBU (WANAOWEZA KUWA BADALA YA MZAZI/MLEZI)**

**NDUGU WA KWANZA:**

1. Jina ..................................................................................................................
2. Simu



Edit with WPS Office

yake.......................................................................................................................

3. Uhusiano na mwanafunzi.................................................................................................

4. Uhusiano wake na mzazi.............................................................................................

**NDUGU WA PILI:**

1. Jina.........................................................................................................................

   simu yake.......................................................................................................................

2. Uhusiano wake na mwanafunzi

   ..........................................................................................

3. Uhuhusiano wake na mzazi..........................................................................................

**Jina la mzazi/mlezi..........................................................................................................**
**.**



Edit with WPS Office